

Bwana aliposema “sikuja kutangua torati bali kuitimiliza” alikuwa
anamaanisha nini?

*Mathayo 5:17 “Msidhani ya kuwa nalikuja KUITANGUA TORATI AU
MANABII; La!, SIKUJA KUTANGUA, bali KUTIMILIZA.*

18 Kwa maana, amin, nawaambia ,Mpaka mbingu na nchi
zitakapoondoka,yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka ,hata
yote yatimie”.

JIBU: BWANA aliposema hakuja kuitangua torati wala manabii bali
kuitimiliza...alikuwa ana maana kuwa yeye hakuja kuondoa neno lolote
la torati lililosemwa bali alikuja kulifanya kuwa **IMARA ZAIDI**..kwa
mfano torati iliposema usizini, haikuishia pale tu katika mwili...lakini
Bwana Yesu alipokuja alisema amtazamaye mwanamke kwa kumtamani
amekwisha kuzini naye nafsini mwake...si umeona hapo.. hajaiondoa
amri ile bali ndio ameikolezea..Ikiwa na maana sio tu kwenda kuchukua
hatua ya kuzini ndio iwe kosa hapana bali kitendo cha kumtamani tu
tayari ni kosa, hivyo haupaswi kutamani kabisa ili kuitimiliza torati...

Kadhalika Torati pia ilisema usiue..lakini Yesu alisemaje? amchukiaye
ndugu yake ni sawa na muuaji..umeona na hapo pia sio tu Kuua ndio iwe
kosa, hapana! bali hata hilo wazo la kumchukia tu ndugu yako halitakiwi

Bwana aliposema “sikuja kutangua torati bali kuitimiliza” alikuwa
anamaanisha nini?

liwepo ndani ya mtu. Torati ilisema pia ikumbuke siku ya sabato uitakase, lakini Bwana Yesu alisema ..Yeye ndiye BWANA wa Sabato (*Marko 2:28*), ikimaanisha kuwa ukimpata Yesu umeishika sabato yako, kwasababu ndani ya moyo wako kila wakati unakuwa ndani ya pumziko lako na kila siku unakuwa katika ibada na sio tena siku moja maalumu.

(*Mathayo 11:28*)...Unaona hapo? Hajaiondoa lakini ameifanya ieleweweke zaidi. Na ndivyo ilivyo pia kwa maneno mengine yote yote ya torati Bwana hakuyaondoa bali aliyafanya kuwa imara zaidi.

Ubarikiwe sana **.jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa**

>> [WHATSAPP](#)

Kwa njia ya maelezo unaweza kufungua video chini

[embedyt] <https://www.youtube.com/watch?v=RxbUfwts4fg>[/embedyt]

Mada zinazoendana:

UTIMILIFU WA TORATI.

Bwana aliposema "sikuja kutangua torati bali kuitimiliza" alikuwa
anamaanisha nini?

JE! VITABU VYA BIBLIA VILIWEZAJE KUKUSANYWA PAMOJA?

UMEIZALIA MATUNDA MIAKA 4 YA NEEMA ULIYOPERA?

USIMFANYIE JEURI ROHO WA NEEMA.

JE! UKRISTO UNAMPA MTU DHAMANA YA KUWA TAJIRI?

TAFUTA KUMJUA MUNGU ZAIDI YA SHETANI

NITASHINDAJE HALI YA KUUMIZWA NA MANENO YA WATU!

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp